

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA

SHULE YA SEKONDARI MARA
S.L.P.193
MUSOMA.

E-mail address: mara.secondary@yahoo.com

Kumb. Na.MSS/SA/50/4/VOL.IV/...

Namba ya simu.

Mkuu wa Shule:**0692 108 218/0763 274 107**

Makamu Mkuu wa Shule:**0759037824/0784729764**

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi:

.....

S.L.P.

.....

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA
SEKONDARI MARA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA
MKOA MARA MWAKA 2018/2019:

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiungana Kidato cha **Tano** katika shule hii mwaka 2018/2019 tahasusi ya Shule ya Sekondari **MARA**. Shule ipo umbali wa kilometa 2 kusini mwa katikati ya mji wa Musoma. Kutoka kituo kikuu cha mabasi cha Bweri, shule iko umbali wa kilometa 9 magharibi. Usafiri ni wa Daladala Tsh. 400/= hadi Musoma basi, kisha Bodaboda ya pikipiki Tsh. 1,000/= hadi shuleni. Endapo utakwenda hadi katikati ya mji, utachukuwa usafiri wa Bodaboda Tsh. 1,000/= hadi shuleni.

Muhula wa masomo utanza tarehe 02/7/2018. Mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **02/7/2018**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **16/7/2018**. Endapo **mwanafunzi atachelewa kuripoti kwa zaidi ya siku 14 kuanzia tarehe ya kufunga shule, nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine.**

Mambo muhimu ya kuzingatia:

2.1: Sare ya shule:

- a) Sare ya shule hii ni suruali mbili nyeusi na mashati mawili meupe mikono mifupi. Suruali lazima iwe na upana wa sm 18 chini na shati lenye upana wa wastani.

Surualiza modo na shati za kubana hazitakubalika.

- b) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
- c) Soksi nyeusi jozi mbili
- d) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali
- e) Sweta moja rangi ya kahawia (zinapatikana shuleni) kwa Tsh. 15,000/=
- f) T-shirt na bukta kwa ajili ya michezo (**rangi ya njano**)
- g) Nguo za kushindia shuleni nje ya masaa ya masomo. Suruali nyeusi mbili na T-shirt mbili za rangi ya bluu zenye kola nyeusi shingoni. T-shirt mbili zinapatikana shuleni kwa Tsh. 20,000/=

NB: Mwanafunzi haruhusiwi kuja shuleni na nguo za nyumbani. Atakayekaidi agizo hiliakaja na nguo hizo, Uongozi wa shule utazikusanya na kuzipeleka katika kituo cha Watoto yatima kilichoko Manispaa ya Musoma kama msaada kwao.

h) **Nywele ziwe fupi** kwa kimo cha nusu sentimeta. Wanafunzi hawaruhusiwi kunyoa **KIPARA**. Endapo mwanafunzi atanyoa kipara atapewa adhabu ya kusimamishwa masomo kwa muda hadi nywele zitakapoota.

i) Kila mwanafunzi ni lazima ahudhuri **parade na Roll call** za kila siku. Mwanafunzi atakaekaidi ataadhibiwa vikali na uongozi wa shule hata kusimamishwa masomo (**SUSPENSION**) na endapo atarudia atafukuzwa shule kabisa.

j) **Simu za mkononi HAZIRUHUSIWI shuleni hapa, mwanafunzi akikamatwa anamiliki simu atafukuzwa shule.**

2.2: Ada na michango ya Shule:

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh.70,000/=. Unaweza kumlipia mwanafunzi Tsh.35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule **Na. 3031200288** katika Benki ya NMB kwenye Tawi lolote hapa Nchini. Tafadhali andika jina kamili la mwanafunzi uliyemlipia pamoja natahasusi (Combination) aliyochaguliwa, kwenye pay in slip.

b) Michango inayotakiwa kulipwana kila mzazi/mlezi ni:

- i) Tsh. 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
- ii) Tsh. 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
- iii) Tsh. 20,000/= kwa ajili ya Taaluma
- iv) Tsh. 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
- v) Tsh. 2,000/= nembo ya shule
- vi) Tsh. 10,000/=; huduma ya kwanza Tsh.5,000/= na Bima ya Afya Tsh.5,000/=

NB: Wanafunzi watashauriwa kujiungana mfuko wa Bima ya Afya kikaya.

- vii) Tsh.20,000/= mitihani ya kujipima (Mock Examination)
- viii) Fedha ya Tahadhari Tsh.5,000/= (**haitarejeshwa**)
- ix) Tsh. 10,000/= dawa ya kunguni kwa mwaka

NB: Jumla ya Ada na michango yote kwa mwanafunzi ni **Tsh.188,000/=** kwa mwaka.

Fedha ya ukarabati pamoja na michango mingine zilipwe kwenye akaunti ya shuleNa.**30301100042NMB**. Risiti za malipo zikabidhiwe wakati wa kuripoti ili mwanafunzi aweze kusajiliwa.

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni:

i) Ream mbili (2) size A4 (Double A)ya karatasi kwa mwaka

ii) Vitabu vya masomo ya Tahasusi (combination) husika.

iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa somola Biology

iv) Scientific calculator

v) Godoro la ft 2½

vi) Shuka pea 2 (rangi ya bluu), blanketi 1, mto na foronya 1, chandarua 1

vii) Vyombo vya kulia chakula – sahani, bakuli,kikombe na kijiko

viii) Ndoo moja ya lita 20 yenye mfuniko, kwa ajili ya usafi pamoja na chombo cha kuhifadhia maji ya kunywa

ix) Jembe 1, reki 1 na mti wake, mfagio wa ndani 1, panga 1 na ufagio wa nje 1.

X) Dawa ya chooni ya unga aina ya chlorine (1kg)

NB: Mwanafunzi andae pesa ya kununua kifaa cha usafi kulingana na eneoatakalopangiwa:

Mf. -Akipangiwa kufyeka nyasi, aje na pesa ya kununua kwanja n.k.